



TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI

**TANGAZO KWA UMMA KUHUSU KUANZA KWA MCHAKATO WA
KUCHUNGUZA NA KUGAWA AU KUBADILI MAJINA YA
MAJIMBO YA UCHAGUZI**

Kwa kuzingatia masharti ya ibara ya 75 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ina mamlaka ya kuchunguza mipaka na kuigawa Jamhuri ya Muungano katika majimbo ya uchaguzi.

Hivyo, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 18(1) ya Kanuni za Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi za mwaka 2024, Tume inatoa taarifa kwamba, mchakato wa kuchunguza na kugawa au kubadili majina ya majimbo ya uchaguzi utanza tarehe 27 Februari, 2025.

Mapendekezo ya kugawanywa au kubadilishwa majina ya majimbo yawasilishwe Tume kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa katika kanuni ya 18(3) ya Kanuni za Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, kama ifuatavyo: -

- (i) Mapendekezo yawasilishwe na kujadiliwa katika vikao vya halmashauri;
- (ii) Mapendekezo yajadiliwe katika Kamati ya Ushauri ya Wilaya;
- (iii) Mapendekezo yawasilishwe kwa Katibu Tawala wa Mkoa kwa ajili ya kujadiliwa katika Kamati ya Ushauri ya Mkoa; na
- (iv) Katibu Tawala wa Mkoa awasilishe mapendekezo ya kugawanya au kubadilisha jina la jimbo pamoja na viambatisho vifuatavyo:
 - (a) Muhtasari wa Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa;
 - (b) Muhtasari wa Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Wilaya; na
 - (c) Muhtasari wa kikao cha Baraza la Madiwani.

Vigezo vitakavyotumika katika kugawanya majimbo ni kama ifuatavyo: -

- (i) Wastani wa idadi ya watu, ambapo kwa majimbo ya mijini ni kuanzia wastani wa watu 600,000 na majimbo ya vijijini ni kuanzia wastani wa watu 400,000



(idadi ya watu itakayotumika ni ile iliyotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwa kuzingatia matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022);

- (ii) hali ya kiuchumi ya Jimbo;
- (iii) ukubwa wa eneo la Jimbo husika;
- (iv) Mipaka ya kiutawala;
- (v) Jimbo moja kutokuwa ndani ya wilaya au halmashauri mbili;
- (vi) mpangilio wa maeneo ya makazi ya watu yaliyopo;
- (vii) uwezo wa ukumbi wa bunge;
- (viii) idadi ya Wabunge wa Viti Maalum Wanawake;
- (ix) upatikanaji wa njia za mawasiliano; na
- (x) hali ya kijiografia ya eneo linalokusudiwa kugawanywa.

Maombi yote yawasilishwe kuanzia tarehe 27 Februari hadi tarehe 26 Machi, 2025 kwa anuani ifuatayo:

Mkurugenzi wa Uchaguzi,
Uchaguzi House,
Eneo la Uwekezaji Njedengwa,
Kitalu D, Kiwanja Na.4,
5 Barabara ya Uchaguzi,
S.L.P. 358,
Dodoma.

Aidha, maombi yatakayowasilishwa baada ya tarehe 26 Machi, 2025 hayatafanyiwa kazi.

Imetolewa leo tarehe 26/2/2025 na:


Kallima, R. K.

MKURUGENZI WA UCHAGUZI

